**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**

SHULE YA SEKONDARI UDEKWA,
S.L.P. 135,
**MAZOMBE.**

KUMB. KDC/UDSS/JI/2021 30/11/2020

**JINA LA MWANAFUNZI.......................................**

**YAH : MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI UDEKWA, WILAYA YA KILOLO, MKOA WA IRINGA MWAKA 2021**

1. **UTANGULIZI**:
Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Udekwa iko umbali wa KM 60 kutoka mji mdogo wa Ilula ulio kwenye barabara ya Dar es salaam – Mbeya. Usafiri wa basi au noah unapatikana kwa nauli ya Tshs 10,000/= ukianzia Ilula. Muhula wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/1/2021 ndani ya siku saba.

2. **MAMO MUHIMU YA KUZINGATIA**

(a) **Sare za shule**
**Wasichana**
Sketi 2 rangi ya udongo (esteem) upana wa mkanda nch 2, marinda 8 ya kupanga, uwe ndefu kuvuka magoti, mashati 2 meupe mikopo mifupi, soksi 2 nyeupe, viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba jozi mbili na sweta la kijani (jani la mgomba).
**Wavulana**
Suruali 2 rangi ya udogo (esteem) marinda mawili kila upande na mkunjo chini (turn up), mashati 2 meupe mikono mifupi, soksi 2 nyeupe, viatu vya ngozi vya kufunga na kamba jozi 2, na sweta la kijani (jani la mgomba) na mkanda wa ngozi mweusi.

(b) Sare za shule za michezo – Kila mwanafunzi awe na raba za michezo, nguo za michezo/truck suit/bukta nyeusi zenye miraba mieupe.

(c) Vifaa vya taaluma – kila mwanafunzi anapaswa kuwa na daftari kubwa (12) kwa kuanzia, karamu za kutosha, rula na mkebe wa hesabu na begi la daftari.

(d) Shule hii ni ya kutwa kwa wavulana, kwa wasichana watakaohitaji kukaa shuleni kuhakikisha mwanafunzi anakua na chakula, nauli ya kuja na kurudi nyumbani, huduma za afya (aje na kadi ya CHIF), pesa ya matumizi (poket money) na mahitaji mengine ya kibinadamu. Kwa wasichana watakao hitaji kukaa hostel (daharia) utaratibu na mahitaji ya daharia vimefafanuliwa kwenye kiambatanisho 01.

3. **SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII**
Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi wa Elimu. unatakiwa kuzingatia.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
(d) Kuwahi katika kila katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule za kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za umama

**MATOKEO YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yote ya kulevya.
v. Makosa mengine ya jinai.
vi. Kupigana na kupiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi.
vii. Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
viii. Kudharau Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
ix. Kuoa au kuolewa.
x. Kupata miomba au kusababisha mimba ndani ya nje ya shule.
xi. Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
xii. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
xiii. Kukataa adhabu halali.
xiv. Kufanya jaribio lolote au kutishia kujiua au kutishia kujiua.
xv. Kufanya jaribio lolote au kutishia kujiua.
xvi. Kumiliki au kukutwa na simu ya mkononi.

4. **MAMBO MENGINE YANAYOPASWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**
   (a) Medical Examination Form – Ijazwe na Mganga Mkuu wa hospital ya serikali na kukabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
   (b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
   (c) Kivuli (copy) cha cheti cha kuzaliwa
   (d) Ream moja (01) ya karatasi
5. Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA UDEKWA SEKONDARI

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI UDEKWA
S.L.P. 135
MAZOMBE-KILOLO

.........................................
ERNEST L. SAKAFU
MKUU WA SHULE

NB : KIKAO CHA WAZAZI WOTE NI TAREHE 15/01/2021 SAA 3:00 asubuhi Udekwa Sekondari.

PRESIDENTS OFFICE (RALG)
KILOLO DISTRICT COUNCIL

UDEKWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 135 MAZOMBE
EDUCATION IS A RESOURCE

TO THE MEDICAL OFFICER
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………
RE……………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………
Please examine the above named person as his/her fitness to studies in the school
EYE……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
EARS…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
CHEST………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……
SPLEEM……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
.
STOOL………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
URINE………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
………
BLOOD………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
MEDICAL CERTIFICATE
I haveexamine the above named person, and considered that;
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
…….
Date …………………………………………………… Signature ……………………………
Hospital/Health centre ……………………………………………………………………
Designation ……………………………………………………

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

SHULE YA SEKONDARI UDEKWA
S. L. P 135,
**MAZOMBE**

MZAZI/MLEZI WA ..........................................................................................

**YAH: KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YALIYOTOLEWA NA SHULE**

Mimi ...................................................................................................

Mzazi/mlezi wa ..........................................................................................

(mwanafunzi) nimesoma sheria, kanuni na maelekezo mengine ya kujiunga na shule ya sekondari Udekwa na ninakubaliana nayo.Pia nimesoma pamoja na mwanangu sheria na kanuni za shule nakiri kuwa nimeelewa.

Jina la mzazi ....................................................... sahihi

....................................

Anuani ya sasa

..............................................................................................

Namba ya simu ...............................................

Jina ia

mwanafunzi...............................................sahihi................................

Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule mwanafunzi anaporudi.

*Kiambatanisho 01*

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**

UDEKWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 135
MAZOMBE
EDUCATION IS A RESOURCE

## UTARATIBU NA MAHITAJI MUHIMU YA DAHARIA (HOSTEL)

Shule ya sekondari Udekwa ina huduma ya hostel kwa wasichana watakaohitaji kukaa shuleni, mahitaji muhimu ya daharia ni kama ifuatavyo;

1. Kila mwana hostel aje na mashuka (2) ya pink, blanketi 1, mto 1, godoro ft 2 x 6, kindoo kimoja cha lita 10 na tochi, Pia vifaa vya chakula kama sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
2. Awe na vifaa binafsi vya usafi kama sabuni za kutosha, mafutKa ya kupaka, mswaki, ndala na mahitaji mengine ya mtoto wa kike.
3. Sare baada ya masomo ni gauni la satini rangi ya damu mzee, mshono wowote wa heshima.
4. UCHANGIAJI WA CHAKULA: Uchangiaji wa chakula unasimamiwa na kamati ya wazazi ya chakula ambayo huchaguliwa na wazazi wenyewe kwenye vikao vya wazazi, mchango wa chakula kwa mwaka ni 380,000 Unaweza kulipa kwa mkupuo au kuchangiua kidogo kidogo kwa awamu nne kwa utaratibu ufuatao;
   - JAN – MARCH 95,000
   - APRIL – JUNE 95,000
   - JULY – SEPT 95,000
   - OCT – DEC 95,000

Michango yote ya chakula ipelekwe benk akaunti ya hostel NMB ILULA, Jina la akaunti ni KMT YA CHAKULA SHULE YA SEK UDEKWA **NO 62810000720**. Mwanafunzi ajapo hostel aje na karatasiu iliyotumika kuweka fedha benk (BPS)

5. Ni marufuku kwa mwanahostel kuja na kisu, simu, kiberiti au mshumaa.

ASANTE

.......................................................................

MKUU WA SHULE

KNY; KAMATI YA UENDESHAJI HOSTEL

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI UDEKWA
S.L.P. 135
MAZOMBE-KILOLO